

3. Animal Farm

3. Animal Farm

Vitabu100Siku100 na Kocha Dr Makirita Amani.

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha tatu kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100. Animal Farm ni riwaya iliyoandikwa na George Orwell kuhusu mapinduzi yaliyofanyika kuondoa uongozi dhalimu lakini mapinduzi hayo yanaleta uongozi mpya ambao ni dhalimu zaidi, huku propaganda zikitumika kuwafanya watawaliwa waone mambo ni mazuri.



Bwana Jones wa shamba la Manor alifunga mabanda ya wanyama akiwa amelewa na kuingia ndani kulala.

Baada ya Jones kwenda kulala, wanyama walio kwenye shamba hilo walikutana, taarifa ilikuwa imesambaa kwamba nguruwe mzee aitwaye Major aliota ndoto ambayo alitaka kuwashirikisha wanyama wengine.

Wanyama wote walikusanyika eneo moja, wakiwepo nguruwe, mbuzi, ng'ombe, kuku, farasi, punda na wengineo.

Baada ya wanyama kufika na kutulia, Major alianza kuwahutumia akiwaita Makomredi.

Anawaambia kabla hajawashirikisha ndoto yake, kuna ujumbe muhimu angependa kuwapatia, maana anajua kwa uzee wake siku siyo nyingi atakufa na hekima hiyo ni muhimu ikawafikia wote.

Major anawaambia wanyama wenzake kwamba baada ya kutafakari kwa kina, jinsi hali ya maisha ya wanyama ilivyo ngumu, wakiwa hovyoy, wakifanyishwa kazi sana na kupata chakula kidogo, amegundua adui mkubwa wa wanyama ni Binadamu.

Anaeleza kwamba binadamu hana anachozalisha, kila kitu anategemea wanyama, kuanzia maziwa, mayai, nyama, ulinzi na hata kazi ngumu.

Anaendelea kueleza kwamba kama wanyama wataweza kumwondoa binadamu, watakuwa huru na maisha yatakuwa mazuri, maana kila wanachozalisha kitakuwa chao.

Major anapendekeza kwamba njia pekee ya kufikia uhuru huo ni kumwondoa mwanadamu, kufanya uasi na kuwaweka wanyama wote huru.

Anawaambia kwamba hilo linaweza lisitokee siku za karibuni, lakini mawazo hayo yaendeleo kukaa kwa kila mnyama, kuna siku yatatimia.

Lakini pia anawatahadharisha wanyama kwamba hata baada ya kumwondoa Binadamu, hakuna mnyama atakayepaswa kuiga tabia za binadamu. Hakuna atakayekaa kwenye nyumba, kuvaa nguo, kunywa pombe, kuvuta sigara, kuwatumikisha wengine, wala kuchukua vitu vya wengine, wanyama wote wanakuwa sawa.

Anaweka msingi kwamba binadamu ndio adui mkuu na wanyama wote ni makomredi.

Chochote kinachotembea kwa miguu miwili na hakina mabawa ni adui, kinachotembea kwa miguu minne au kina mabawa ni rafiki.

Wakati Major anasema hivyo panya wanajitokeza na paka wanataka kuwakamata, anasema hilo siyo sahihi, wanyama wote ni sawa na wanapaswa kuwa na umoja.

Anaitisha kura ya kuamua kama panya ni makomredi au maadui, wanyama wote isipokuwa paka na mbwa wanapiga kura kuwa panya ni makomredi.

Major anamalizia hotuba yake kwa kushirikisha ndoto yake, ambayo ni kumbukumbu ya wimbo wa mapinduzi aliokuwa anaimba akiwa mtoto.

Anaimba wimbo huo na kupokelewa na wanyama wengine, ambao wanauimba kwa hamasa kubwa kitu kinachomfanya bwana Jones aamke na kupiga risasi angani.

Wanyama wote wanatawanyika na kwenda kulala.



2

Siku tatu baada ya mkutano wa wanyama Major anafariki usingizini.

Lakini wanyama wote wamebaki na matumaini makubwa juu ya mapinduzi ya kumwondoa binadamu. Vikao na mafunzo ya siri yanaendelea, nguruwe ndiyo wanapewa jukumu la kuendesha mafunzo hayo.

Nguruwe watatu waitwao Snowball, Napoleon na Squealer ndiyo wasimamizi wakuu wa hilo.

Wanatengeneza mfumo mpya wanaouita Animalism na kuufundisha kwa wanyama wote.

Mwanzo wanakutana na ugumu, wanyama wengi wana wasiwasi iwapo watampindua binadamu, hawataweza kuyaendesha maisha yao wenyewe.

Viongozi hao wanawapa moyo kwamba binadamu akishaondoka, watakuwa huru kuyaendesha maisha yao na kila wanachotaka watapata, bila ya kupangiwa.

Hali ya shamba haiendi vizuri Bwana Jones ameshindwa kesi na hivyo hana fedha za kuliendesha shamba, analewa na hajali tena kuliangalia shamba vizuri.

Siku moja akiwa ameenda kulewa wafanyakazi wake hawakuwalisha wanyama kwa siku nzima, wanyama wanapaswa hasira, wanavunja mazizi yao na kuanza kuwapiga wafanyakazi hao.

Wafanyakazi wanajaribu kuwapiga lakini wanashindwa, wanaamua kukimbia kuokoa uhai wao.

Bwana Jones naye anakimbia. Wanyama hawaamini kilichotokea, mapinduzi yamekamiliwa, binadamu wameondolewa na sasa shamba lote ni mali yao.

Wanalizunguka shamba na kuchoma moto vifaa vyote ambavyo binadamu walikuwa wanatumia kuwatesa navyo, kama visu, kamba, mijeledi n.k.

Wanakubaliana nyumba ya binadamu isiharibiwe, ibaki kama eneo la makumbusho na hakuna mnyama atakayeruhusiwa kuishi huko.

Snowball na Napoleon ndiyo viongozi wakuu, ndiyo wanaojua kusoma na kuandika.

Wanavadili jina la shamba, kutoka MANOR FARM na kuwa ANIMAL FARM.

Pia wanaandika amri saba za mfumo wao wa Animalism ambazo ni;

1. Kiendacho kwa miguu miwili ni adui.
2. Kiendacho kwa miguu minne au chenye mabawa ni rafiki.
3. Hakuna mnyama atakayevaa nguo.
4. Hakuna mnyama atakayelala kwenye kitanda.
5. Hakuna mnyama atakayekunywa pombe.
6. Hakuna mnyama atakayemuua mnyama mwingine.
7. Wanyama wote ni sawa.

Baada ya wote kuelewa amri hizi, wanakubaliana waende kuvuna nyasi. Ng'ombe wanalalamika kwamba hawajakamuliwa kwa siku nzima hivyo maziwa yanawauma.

Nguruwe wanachukua ndoo na kuwakamua, zinapatikana ndoo tano za maziwa na maumivu yanawaisha.

Wanyama wengine wanauliza maziwa hayo yatapelekwa wapi?

Napoleon anawajibu wasifikirie sana hayo maziwa, waende wakavune nyasi, watangulie yeye atakuja.

Wanaenda kuvuna nyasi, ila wanaporudi wanakuta maziwa hayapo.



3

Kazi ya kuvuna nyasi inakuwa ngumu, lakini wanyama wanaifanya kwa moyo na kufanikiwa kupata mavuno makubwa kuliko wakati wa binadamu.

Kila mnyama anafanya kazi kwa uwezo wake, farasi wanajituma zaidi na hata ndege wanatumia midomo yao kufanya kazi.

Nguruwe wanakuwa viongozi, wao hawafanyi kazi za nguvu, badala yake wanaweka mipango na kuwasimamia pamoja na kuwahamasisha wengine.

Snowball anakuwa na mkakati mkali, anaandaa kamati mbalimbali, ziliwepo za elimu.

Wanyama wote wanafundishwa kusoma na kuandika, wanyama wengi wanafanikiwa kujua kusoma na kuandika, lakini wengine wanashindwa.

Nguruwe wanatenga jengo la mavuno kuwa ndiyo makao makuu na ofisi zao.

Siku za jumapili hakuna kazi, wanyama wanaamka asubuhi, wanapandisha bendera yenye rangi ya kijani, kwato na pembe na kuimba wimbo wa mapinduzi.

Baada ya hapo nguruwe wanasoma mpango wa kazi wa wiki inayofuata na kisha watu wanakuwa na mapumziko.

Kwa kuwa baadhi ya wanyama hawajazikariri amri saba za Animalism, Snowball anazirahisisha na kupata kauli moja iliyobeba msingi mzima. Kauli hiyo ni; MIGUU MINNE NZURI, MIGUU MIWILI MBAYA. Ndege wanalalamika kwamba kauli hiyo inawafanya waonekani ni wabaya, wanafafanuliwa kwamba kwa kuwa mabawa yao yanatumika kuruka basi ni miguu na siyo mikono kama ya binadamu ambayo kazi yake ni unyonyaji.

Swali la maziwa yanaenda wapi linapatiwa jibu, nguruwe wamekuwa wanayatumia.

Wanyama wengine wanapolalamika, Squealer anawapa ufafanuzi kwamba nguruwe ndiyo wanaoongoza na kuweka mipango yote, wanahitaji kupata virutubisho ili akili zao ziwe sawa. Kama nguruwe hawatapata virutubisho, watashindwa kuongoza vizuri na bwana Jones atarudi kwenye shamba hilo.

Wanyama kusikia hivyo wanaacha kulalamika, maana hawataki bwana Jones arudi na kukosa uhuru ambao wameshaupata.

Pia Napoleon ana mkakati wa siri, anachukua watoto wadogo wa wanyama na kwenda kuwahifadhi eneo maalumu ambapo wanapatiwa mafunzo maalumu.



Habari za mapinduzi yaliyofanywa na wanyama zinasambaa maeneo mbalimbali.

Snowball na Napoleon wanatuma makundi ya ndege kusambaza taarifa hizo kwenye mashamba jirani, huku wakiwatuma kufundisha wimbo wa mapinduzi.

Bwana Jones amekuwa akilalamika jinsi ambavyo ameondolewa kwenye shamba lake na wanyama wakaidi.

Shamba linaloendeshwa na wanyama limepakana na mashamba mengine mawili ambayo yanamilikiwa na Pilkington na Frederick.

Lakini wamiliki hao wamekuwa hawana maelewano, hivyo hawajaweza kuungana na kukabiliana na wanyama hao.

Ambacho wamekuwa wanafanya ni kuzuia taarifa za mapinduzi hayo zisiwafikie wanyama wao na kukataza wimbo wa mapinduzi usiimbwe.

Lakini pamoja na hayo, bado taarifa zinasambaa kwa kasi na wimbo wa mapinduzi unakuwa maarufu.

Wamiliki wa mashamba jirani wanasambaza propaganda kwamba hali kwenye shamba la wanyama siyo nzuri, wanatesana na kuuana, lakini taarifa hizo kwa awali siyo za kweli.

Bwana Jones anapata watu wa kumuunga mkono na kwa pamoja wanakuja kuwashambulia wanyama ili warudishe shamba.

Kundi la watu wenye fimbo huku Jones akiwa na bunduki wanavamia shamba, lakini Snowball alikuwa ameshapata taarifa na alikuwa amesoma kitabu cha mbinu za kivita za Julius Caesar na kupanga mashambulizi vizuri.

Kunatokea mapigano na wanyama wanafanikiwa kuwashinda binadamu, ambao wanakimbia.

Bunduki ya Jones inabaki, ambayo inawekwa chini ya bendera kama alama ya ushindi.

Wanaandaa tuzo za kivita na kuipa vita hiyo jina, huku siku ya ushindi ikifanywa siku ya kumbukumbu.



Mnyama anayeitwa Mollie amekuwa na tabia zisizoeleweka, mara kwa mara haonekani na hajulikani anakuwa wapi.

Siku chache baadaye haonekani tena, ndege wanasema ameonekana kwenye shamba la jirani akiwa analishwa sukari na binadamu huku akiyafurahia maisha.

Kwenye shamba la wanyama mambo hayaendi vizuri kama awali, kwanza hali ya hewa siyo nzuri, jua ni kali sana.

Pili Snowball na Napoleon wamekuwa hawaelewani, kwenye kila jambo wanabishana na kupingana.

Snowball amekuwa na mikakati mingi ya kuboresha shamba, lakini kila anapoipendekeza, Napoleon anaipinga na kusema haiwezekani, huku yeye akiwa hana mkakati wowote.

Kunatokea mgawanyiko baina ya wanyama, kuna ambao wako upande wa Snowball na wengine upande wa Napoleon kasoro mnyama mmoja, punda mzee aitwaye Benjamin amekuwa hayupo upande wowote na amekuwa anawaeleza wazi wanyama wengine kwamba kwa uzoefu wake, kuwa upande wowote ule hakusaidii chochote, maisha yatazidi kuwa magumu.

Snowball amekuwa na mpango wa kufua umeme wa upepo, amejifunza kupitia vitabu mbalimbali na kuandaa michoro ya jinsi hilo litakamilika.

Anawaalika wanyama kuangalia michoro yake na wengi wanaifurahia, lakini Napoleon tangu mwanzo anapinga mpango huo, anasema kipaumbele kwa sasa ni kuongeza chakula.

Inapangwa ipigwe kura na wanyama wote kama mpango huo upitishwe au la.

Snowball anaelezea mpango huo, anaeleza jinsi utakavyopunguza kazi na kurahisisha maisha.

Snowball ana ushawishi mkubwa na wanyama wanaonekana kumwelewa.

Napoleon anasema mpango huo hauna maana na wanyama hawapaswi kuupigia kura.

Snowball anaendelea kuutetea kwa nini ni mpango sahihi. Mara ghafla Napoleon anapiga mluzi na mbwa wakali wanakuja na kuanza kumfukuza Snowball ambaye anakimbia mpaka kutoka nje ya shamba.

Wanyama wanafadhaishwa na hilo, Napoleon anawaeleza kwamba kuanzia hapo hakutakuwa tena na vikao vya jumapili vya kujadiliana ni upotevu wa muda.

Maamuzi yote yatafanywa na kamati ya nguruwe kisha wanyama watasomewa siku ya jumapili baada ya kupandisha bendera na kuimba wimbo wa mapinduzi.

Watu bado wanajiuliza mbwa wale wametoka wapi, jibu linapatikana, ni watoto wa mbwa ambao

Napoleon alikuwa anawachukua kwa wazazi wao na kwenda kuwalea kwa siri.

Kwa sasa mbwa hao wanaambatana na Napoleon kila mahali, ni wakali na watu wanawaogopa.

Squealer anatumwa kwenda kuwashawishi watu zaidi, anawaeleza kwamba Napoleon anajitoa sana kwa ajili yao, uongozi siyo kazi rahisi na Snowball alikuwa msaliti ndiyo maana imebidi afukuzwe.

Wiki tatu baada ya Snowball kufukuzwa shambani, Napoleon anatangaza kwamba mfumo wa umeme wa upepo utajengwa, hakuna maelezo ya ziada yanayitolewa.

Squealer anaeleza kwamba mpango huo ulikuwa wa Napoleon tangu awali, ila Snowball aliuiiba ili ajipatie sifa. Hivyo Napoleon aliona ni bora Snowball aondolewe kwanza kwa sababu ni msumbufu.



Kazi zinakuwa ngumu kwenye shamba la wanyama, lakini wanazifanya kwa moyo na kujituma.

Ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa jua unaendelea, kazi ni ngumu lakini wanyama wanajituma zaidi.

Inagundulika kwamba wanyama hao watahitaji vitu zaidi ili kukamilisha ujenzi huo, vitu ambavyo hawawezi kutengeneza wenyewe.

Napoleon anawatangazia kwamba itabidi washirikiane na binadamu, wawauzie baadhi ya vitu ili waweze kupata fedha za kununua mahitaji wanayotaka.

Anawaambia wanyama wasijali, wao hawatakutana na binadamu, ila yeye ndiye atakayefanya hivyo.

Amechagua mtu mmoja ambaye ndiyo atakuwa kiungo kati ya wanyama na binadamu.

Wanyama wanakuwa na minong'ono, moja ya amri zao ni kutokushirikiana na wanadamu au kujihusisha na fedha.

Squealer anawaambia siyo kweli, amri hazijasema hivyo, watakuwa walielewa vibaya. Anawauliza kama wana mahali wameandika, wanamjibu hakuna na kukubaliana naye kwamba watakuwa walielewa vibaya.

Inatangazwa kwamba nguruwe watahamia kwenye nyumba ya wanadamu kwa sababu wana kazi nyingi za kutumia akili za kufanya, wanahitaji eneo tulivu.

Wanyama wanakuwa na minong'ono pia, amri zilikataza kukaa kwenye nyumba na kulala kwenye vitanda.

Mnyama mmoja anayekubuka zilipoandikwa amri anaenda kuzisoma lakini haoni vizuri, anaita

mnyama mwingine amsaidie kusoma amri ya nne, ambayo inasomeka; hakuna mnyama atakayelala kwenye kitanda chenye mashuka.

Wakiwa hapo Squealer anapita, anawaambia wamejionea wenyewe amri inavyosema na katika kuitimiza, nguruwe wameondoa mashuka yote kwenye vitanda na kuacha mablanketi.

Anaendelea kuwasisitiza wanyama kwamba kama viongozi hawatapata utulivu na kuongoza vizuri, bwana Jones atarudi, je hicho ndiyo wanataka?

Wanyama wanajibu hapana, hawataki kabisa Jones arudi.

Uskiku mmoja kunakuwa na upepo mkali na sauti za vishindo. Wanaamka asubuhi na kukuta mtambo wa kufua umeme wa upepo waliojenga umebomoka wote.

Napoleon anatangaza kwamba aliyefanya uharibifu huo ni Snowball, msaliti ambaye hataki wanyama hao waendeleo.

Anatangaza zawadi nono kwa atakayemkamata na kumleta Snowball.

Pia anatangaza ujenzi wa mtambo huo kuanza upya na hauka kitakachowazuia ije mvua au jua.



Hali ya hewa ni mbaya, baridi ni kali lakini wanyama wanajituma kujenga mtambo wa kufua umeme. Hawataki kuchelewa kuukamilisha kwa sababu wanadamu wamekuwa wanasema hautakamilika, hivyo wanataka kuonesha wanakosea.

Wanadamu wamekuwa wakieleza kilichosababisha mtambo huo kuanguka ni kuta kukosa uimara, wanyama wanasisitiza Snowball ndiyo aliyuharibu, hapo sasa wanajenga ukuta imara zaidi.

Hali ya chakula pia siyo nzuri, hakipo cha kutosha, hivyo mgao wa chakula unazidi kuwa mkali kwa kiwango kupunguzwa.

Wanadamu wanaendelea kusambaza taarifa kwamba shamba la wanyama lina njaa na wanyama wanakufa.

Napoleon anatengeneza picha ya kumfanya mwanadamu anayekuja kwenye shamba hilo kuona kwamba kuna chakula. Anaagiza ndoo ziwekwe mchanga kisha huu pawekwe nafaka, kitu kinachomwaminisha mwanadamu kwamba shamba hilo lina chakula cha kutosha.

Napoleon anawaeleza wanyama kwamba wanapaswa kujitoa zaidi ili kukamilisha mtambo.

Anawaambia kuku wawe tayari kutoa mayai zaidi.

Kuku wanagoma na kusema kama mayai yao yote yatachukuliwa, hawataweza kuzaliana.

Wanaamua kupanda juu ya paa na kutaga ili mayai yavinjike. Napoleon anatangaza kuku wasipewe chakula kabisa na mnyama yeyote atakayekamatwa anawapa chakula aadhibiwe kifo.

Baada ya siku chache kuku wanasalimu amri na kuachana na mgomo wao.

Kila kibaya kinachofanyika kwenye shamba la wanyama, kila kinachopotea au kukosekana, lawama zinaenda kwa Snowball.

Squealer anawaambia wanyama kwamba imegundulika Snowball alikuwa upande wa Jones tangu awali na hata siku ya uvamizi, Snowball alikuwa anahujumu upande wa wanyama ushindwe na isingekuwa Napoleon, siku ile wanyama wangeshinda.

Wanyama wanalikataa hilo, wanasema Snowball alipambana sana mpaka akaumia, haiwezekani alikuwa upande wa Jones.

Squealer anawaambia Napoleon ameona nyaraka za siri ambazo Snowball aliandika mwenyewe.

Wanyama kusikia Napoleon amesema hivyo, wanakubali maana wanaamini Napoleon huwa yuko sahihi.

Siku moja Napoleon anaitisha mkutano wa wanyama wote, anawasili akiwa amezungukwa na kundi la mbwa.

Anapiga mluzi na mbwa wanaenda kuwakamata nguruwe wanne na kuwaleta mbele, Napoleon anawaambia wakiri makosa yao, wanaeleza kwamba wamekuwa wanashirikiana na Snowball kulihujumu shamba hilo. Baada ya kukiri wanakatwa shingo.

Kuku walioanzisha mgomo nao wanatoka kukiri walishawishiwa na Snowball, nao wanakatwa shingo.

Zoezi hilo linaendelea na wanyama wengi wanapoteza uhai wao.

Baada ya zoezi hilo wanyama wanabaki na simanzi kubwa, hawajawahi kuona kitu kama hicho, hata

wakati wa Jones.

Tangu mapinduzi yametokea, hakuna mnyama amewahi kumuua mnyama mwingine.

Wanatafakari ndoto walizokuwa nazo wakati wa mapinduzi na kuona ni tofauti kabisa na kinachotokea sasa.

Kwa pamoja wanaimba wimbo wa mapinduzi kwa majonzi makubwa.

Wakiwa wanaimba Squealer anakuja mbio na kuwaambia Napoleon amepiga marufuku kuibwa kwa wimbo huo.

Wanyama wanashangazwa na kuuliza kwa nini, Squealer anawajibu mapinduzi yalishafanyika na yamefanikiwa, wasaliti wote wameondolewa hivyo wimbo huo hauna umuhimu tena.

Unatungwa wimbo mwingine mfupi wa kusifia shamba la wanyama na huo ndiyo unakuwa unatumika.

👉8

Baada ya kukiri na kuuawa kwa wasaliti, wanyama wanakumbuka kwamba kulikuwa na amri inayozuia wanyama wasiue wanyama wengine.

Wanaenda kusoma amri hiyo ya sita na kukuta imeandikwa hakuna mnyama atakayemuua mnyama mwingine bila sababu.

Na hapo wanaona wao ndiyo hawakuwa wameelewa, kwani waliouawa kulikuwa na sababu, walikuwa wasaliti.

Kazi zinazidi kuwa nyingi na ngumu ujenzi wa mtambo wa kufua umeme unandelea na wanyama wanajituma kwa moyo wote.

Napoleon amekuwa haonekani kama zamani, anaonekana mara chache na anakuwa ameambatana na mbwa wakali.

Maagizo yote yanatolewa na Squealer, Napoleon anapewa heshima na utukufu mkubwa, akiitwa 'Kiongizi wetu Komredi Napoleon'

Anapewa majina ya ziada kama baba wa wanyama wote, hofu ya binadamu, mlinzi wa kondoo, rafiki wa ndege n.k.

Siku yake ya kuzaliwa inafanywa kuwa sikukuu.

Kila mafanikio yanayopatikana sifa zinaenda kwa Napoleon hata kama hahusiki. Mfano kuku walisikika wakisema 'chini ya uongozi mzuri wa kiongozi wetu Komredi Napoleon nimetaga mayai matano kwa siku sita.'

Kupitia mtu wa kati ambaye Whymper, Napoleon alikuwa anajadiliana na wamiliki wawili wa mashamba, Frederick na Pilkington kuhusu kuwauzia mbao.

Ilionekana Pilkington ndiyo mwenye maelewano mazuri huku Frederick akisemekana ni katili na anayetesa wanyama.

Lakini mwisho wa siku Frederick ndiye anauziwa mbao, analipa fedha lakini zinakuja kusemekana ni fedha bandia.

Frederick na watu wake wanalivamia shamba la wanyama, wanalipua mtambo wa kufua umeme wa jua ambao ulikuwa umekamilika.

Hilo linawapa hasira kali wanyama na kwenda kuwakabili bila hofu, licha ya kuwa na bunduki.

Wanyama wengi wanakufa kwenye pambano hilo, ila mwishi wanadamu wanakimbia.

Mtambo umeharibiwa kabisa na wanyama wengi wamekufa huku wengine wakibaki na majeraha.

Napoleon anatangaza wamepata ushindi mkubwa, lakini wanyama hawaelewi, ushindi gani wakati mtambo umeharibiwa na wanyama wamekufa? Lakini hilo halizuii sherehe za ushindi ambapo zimetengwa siku 2.

Usiku mmoja wanyama wanasikia kishindo kikubwa, wanatoka nje na kumkuta Squealer akiwa chini ya eneo zilipoandikwa amri, ngazi imevunjika na ana rangi na brashi ya kuandika. Mbwa wanamfuata na kumpeleka ndani.

Wanyama wanasogelea zilipo amri na wanasoma amri ya tano, ambayo awali walijua ilisema hakuna mnyama atakayekunywa pombe, lakini sasa inasomeka hakuba mnyama atakayekunywa pombe kupitiliza.

Wanyama wanajiambia walielewa vibaya au kusahau.



9

Wanyama wanaamua kujenga upya mtambo wa kufua umeme ulioharibiwa. Kazi zinakuwa nyingi na wanyama wameumia, lakini wanajisukuma kufanya. Sehemu ya shamba imetengwa kwa ajili ya kulima shayiri na eneo la kutengeneza pombe ambalo liliachwa na Jones limeanza kutumika. Nguruwe wameanza kuzalisha pombe ambayo wanatumia wao tu. Maelekezo yanatolewa kwamba nguruwe ndiyo daraja la juu na mbwa wanafuatia. Wanyama wengine wanapokutana na nguruwe au mbwa njiani, wanapaswa kuwapisha. Nguruwe wanazaliana kwa wingi na Napoleon anaweka mpango wa kujenga madarasa ili watoto wa nguruwe wapate elimu. Hilo linafanya kazi kuwa nyingi zaidi, huku maisha yakiwa magumu kwani mgao wa chakula umezidi kuwa mkali, kiwango kimepunguzwa zaidi. Kila siku Squealer anawasomea wanyama ongezeko la uzalishaji ambalo limefikwa na wanyama wanaamini maana hawana njia ya kupima. Anazidi kuwasisitiza kwamba hali waliyonayo sasa ni nzuri ukilinganisha na kipindi wako chini ya Jones. Siku moja farasi ambaye amekuwa anajituma sana kwenye kazi alianguka na kushindwa kuinuka. Farasi huyo aitwaye Boxer amekuwa anafanya kazi kupitiliza, kauli mbiu zake kuu ni 'nitafanya kazi zaidi' na 'Napoleon yuko sahihi mara zote.' Squealer anapewa taarifa ya Boxer kuanguka na kuja akiwaambia wanyama kwamba Napoleon amesikitishwa sana na hali iliyomkuta mnyama mtiifu Boxer na atapelekwa mjini kwa daktari wa wanyama. Wanyama wanakuwa na wasiwasi na hilo, wakitaka atibiwe hapo shambani, lakini Squealer anawaambia hakuna matibabu mazuri kwake. Gari inakuja kumchukua Boxer, wanyama wanakusanyika kumuaga, punda mzer Benjamin anawaambia waache ujinga, wasome gari imeandikwaje, anawasomea, ni gari la machinjio ya farasi. Wanyama wanajaribu kuzuia lakini wanakuwa wameshachelewa, gari imeondoka. Siku chache baadaye Squealer anawapa taarifa kwamba Boxer amefariki dunia akipatiwa matibabu na yeye alikuwepo wakati anakata roho. Anaeleza amesikia tetesi kwamba watu wanaamini Boxer alienda kuchinjwa, anawaambia gari ile ilinunuliwa na hospitali ya wanyama na bado hawajaibadili jina. Wanyama kusikia hivyo wanaridhika na kuondokwa na wasiwasi. Napoleon anamuenzi Boxer na kuwataka wanyama wote kuishi kwa misingi aliyoiishi Boxer.



10

Miaka mingi inapita na wanyama waliokuwepo wakati wa mapinduzi wengi wameshakufa. Walio hai ni watatu, punda mzee Benjamini, farasi Clover na kunguru Moses. Kizazi kipya cha wanyama hawajui mambo yalivyokuwa awali na pia ni rahisi kudanganyika na kuamini chochote wanachoambiwa na nguruwe. Kwa ujumla shamba linaendeshwa kwa mafanikio makubwa, mtambo wa kufua umeme umekamilika na umeshaanza kutumika. Nguruwe na mbwa ndiyo wako kwa wingi na hao hawafanyi kazi yoyote ya uzalishaji. Licha ya shamba kuwa na mafanikio, wanyama wengine hali zao bado siyo nzuri, wanafanyishwa kazi muda mrefu huku chakula wanachopewa ni kidogo. Kwa kuwa wengi hawajui maisha ya awali, wanaona ni sawa tu. Punza mzee Benjamin bado ana msimamo wake kwamba hakuna ambacho kimewahi kuwa bora na wala hakuna kitakachokuja kuwa bora, hali itaendelea hivyo tu. Shamba la wanyama limekuwa jamhuri na raisi ni Napoleon ambaye hajawahi kuwa na mpinzani. Siku moja Squealer anawaita kondoo wote na kuwapeleka eneo la siri na kisha kukaa nao hapo. Kwa wiki nzima kondoo hawaonekani, Squealer anaeleza wanapewa mafunzo ya wimbo maalumu. Baada ya wiki kuisha, kondoo wanarudi kwenye maisha ya kawaida.

Sauti inasikika ikiwaita wanyama wengine, ni Clover anaita wanyama waje wajionee. Wanafika na kuona msafara wa nguruwe wakitoka ndani ya nyumba kwakitembea kwa miguu miwili. Clover anashangazwa na hilo, maana anajua moja ya amri zao ni MIGUU MINNE NZURI, MIGUU MIWILI MBAYA.

Kabla hawajafanya chochote, kondoo wanasikika wakiomba 'Miguu minne nzuri, miguu miwili bora.' Clover anamtaka Benjamin waende palipoandikwa amri saba, wanafika pale na kukuta amri zimefutwa na kuna kauli moja inayosema; WANYAMA WOTE NI SAWA, LAKINI BAADHI YA WANYAMA NI BORA KULIKO WENGINE.

Tangu hapo mambo yakawa yamebadilika kabisa, nguruwe wote wanatembea kwa miguu miwili, wanasimamia wanyama wengine kwa kutumia mijeledi, wanavaa nguo, wanavuta sigara na mengine yaliyokuwa yanafanywa na binadamu.

Siku moja kundi la watu wanatembelea shamba lao, wanapokelewa na nguruwe na kuzungushwa kwenye shamba. Mwisho wanakaribishwa ndani ya nyumba.

Wanyama wanasikia kelele za vicheko na furaha vikitoka ndani ya nyumba ile.

Wanasogea kuchungulia, wanakuta watu na nguruwe wamekaa mezani, huku wakila na kunywa pombe kwa furaha.

Bwana Pilkington anasimama kuongea na kusema anashukuru uhasama baina ya mashamba hayo umeisha na sasa wanaweza kushirikiana.

Anamsifu Napoleon kwa uongozi wake mzuri, ambapo ameweza kuwabana wanyama wa hadhi ya chini na kuleta uzalishaji mkubwa, huku wakilishwa kidogo. Ni kitu anachoahidi kuiga na kwenda kutekeleza kwenye mashamba yao.

Napoleon naye anaongea kushukuru kwa ushirikiano huo na kusema kuna mabadiliko kadhaa yatafanyika, bendera itaondolewa pembe na kwato na kubaki jina tu na hata jina la shamba, halitakuwa tena Animal Farm, badala yake litarudi kuwa jina lake halisi Manor Farm.

Wanyama waliokuwa wanachungulia dirishani wanapatwa na bumbuwazi, wanajaribu kuwaangalia nguruwe, kisha wanawaangalia binadamu na wanarudi tena kuwaangalia nguruwe na wanaona hakuna tofauti yoyote.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,
www.t.me/somavitabutanania